


Nation Printers and Publishers Limited

CMA-LIBRARY



CMA-LIBRARY


DT
448.2
K46
N385
1994
C-1

[illegible]

Nation Printers and Publishers Limited

CMA-LIBRARY

CMA-LIBRARY



CMA - Ke Library



AR0244

The hand is perhaps the most expressive feature of the human personality. It indicates sensitivity, strength, compassion, action, character and emotion; all elements reflective of a responsive newspaper.

We believe that at Nation we have combined professional journalism with a strong sense of social commitment arising out of many years of "Hands - On" experience.

A. Poomawala



W. Robinson



G. M. Wilkinson



H. H. O. Awori



Dr. B. M. Gecaga, C.B.S.



S. A. Martin



A. A. A. Ekirope



W. D. Kiboro




DT
448.2
• 1246
N 385
1954
C.1
3

1. Median media group - pendulum
2. Median group - pendulum

Board of Directors		Halmashauri ya Wakurugenzi
Chairman (Kenyan)	A. A. A. Ekirapa	<i>Mwenyekiti (Mkenya)</i>
Managing (Kenyan)	W. D. Kiboro	<i>Msimamizi (Mkenya)</i>
(Kenyan)	H. H. O. Awori	<i>(Mkenya)</i>
(Kenyan)	Dr. B. M. Gecaga, C.B.S.	<i>(Mkenya)</i>
(British)	S. A. Martin	<i>(Mwingereza)</i>
(French)	A. Poonawala	<i>(Mfransa)</i>
(Australian)	W. Robinson	<i>(Mwa—Australia)</i>
(Irish)	G. M. Wilkinson	<i>(Mwa—Irish)</i>
Secretary	S. G. Ogutha, CPA(K), CPS(K)	<i>Katibu</i>
Registered Office	Nation Centre Kimathi Street Nairobi	<i>Afisi Iikoandikishwa</i>
Bankers	Standard Chartered Bank Kenya Limited Moi Avenue Nairobi	<i>Benki</i>
Auditors	Coopers & Lybrand Kaunda Street Nairobi	<i>Wakaguzi wa Hesabu</i>
Subsidiary Companies	Nation Newspapers Limited Nation Marketing & Publishing Limited Nation Carriers Limited Nation Infotech Limited	<i>Makampuni Madogo</i>
Associated Companies	Kenya Litho Limited Industrial Promotion Building Limited	<i>Makampuni yaliyoshirikishwa</i>

Nation ... Accurate ... Authoritative ... Courageous ... Entertaining ... Informative ...
Investigative ... Reliable. **"Hands - On"** news coverage of all aspects of life.



Contents

Yaliyomo

	Page Ukurasa
Board of Directors	3
<i>Halmashauri ya Wakurugenzi</i>	3
Notice of Annual General Meeting	6
<i>Tangazo la Mkutano wa kila Mwaka</i>	7
Directors' Report	8
<i>Taarifa ya Wakurugenzi</i>	9
Chairman's Report	10
<i>Taarifa ya Mwenyekiti</i>	13
Report of the Auditors	17
<i>Taarifa ya Wakaguzi wa Hesabu</i>	17
Profit and Loss Account	18
<i>Hesabu ya Faida na Hasara</i>	19
Balance Sheet	20
<i>Hesabu ya Fedha</i>	21
Source and Application of Funds	22
<i>Mapato na Matumizi ya Fedha</i>	23
Notes to the Accounts	24–34
<i>Maelezo Juu ya Hesabu</i>	25–35

Notice of Annual General Meeting

Notice is hereby given that the Thirty Second Annual General Meeting of the Members of Nation Printers and Publishers Limited will be held at the Hotel Inter-Continental, Nairobi, on Thursday, 15 June, 1995 at 3.00 p.m. for the following purposes:-

- 1 To receive and consider the Accounts for the year ended 31st December, 1994 and the Chairman's, Directors' and Auditors' Reports thereon.
- 2 To confirm the payment of the interim dividend of 12.5% and to approve the payment of a final dividend of 32.5% on the ordinary Share Capital in respect of the year ended 31st December, 1994.
- 3 To consider and, if thought fit, to pass the following resolutions as Ordinary Resolutions:-
 - (a) **TO RESOLVE**, that the authorised Share Capital of the Company be increased from 10,000,000 shares of KShs. 5/- each to 30,000,000 shares of KShs. 5/- each.
 - (b) **TO RESOLVE**, that it is desirable to capitalize a sum of KShs. 11,884,210/- being part of the amount standing to the credit of revenue reserves and accordingly subject to approval by Capital Markets Authority and Central Bank of Kenya that sum be made available for distribution amongst the shareholders of existing Ordinary Shares in the capital of the Company on the condition that the same be not paid in cash but applied in paying up in full at par 2,376,842 shares credited as fully paid up, be accordingly allotted to such shareholders respectively in the proportion of one such new share for every four (4) of the existing 9,507,368 shares then held by such shareholders respectively (fraction of a share to be disregarded) and that the shares so distributed shall be treated for all purpose as an increase of the issued share capital of the company held by each such shareholder and not as income and further that such shares shall rank *pari passu* for all purposes, with the existing shares in the capital of the company with the exception of the final dividend for the year 1994 payable on June 30, 1995 and any other dividend declared prior to the issue of the additional shares and the Directors be and are hereby authorised and directed to give effect to this resolution.
- 4 To authorise the Directors to fix the Auditors' remuneration.
- 5 To elect Directors:
In accordance with Article 96 of the Articles of Association, Mr. W. D. Kiboro retires and, being eligible, offers himself for re-election.

In accordance with Article 110 of the Articles of Association, Mr. A. A. A. Ekirapa, Mr. H. H. O. Awori and Mr. W. Robinson retire by rotation. Mr. Awori and Mr. Robinson, being eligible, offer themselves for re-election. Mr. Ekirapa is not seeking re-election.

- 6 To transact any other competent business.

Note:

A member entitled to attend and vote may appoint a proxy to attend and vote for him on his behalf. Such Proxy need not be a member of the Company. To be valid, Proxy Forms must be deposited at the Company not less than 48 hours before the appointed time of the meeting.

By Order of the Board
S.G. Ogutha
Secretary

23rd March, 1995

Tangazo la Mkutano Mkuu wa kila Mwaka

Notisi inatolewa hapa kwamba Mkutano mkuu wa kila mwaka wa Thelathini na Mbili wa Wanachama wa Nation Printers and Publishers Limited utafanywa hoteli ya Inter-Continental, Nairobi, Alhamisi, Juni 15, 1995, saa tisa za mchana, kwa shughuli zifuatazo:-

- 1 Kupokea na kujadili Hesabu za mwaka uliomalizikia Desemba 31, 1994 na Ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi wa Hesabu.
- 2 Kuthibitisha ulipaji wa mgawo wa muda wa asilimia 12.5 na kuidhinisha malipo ya mwisho ya mgawo wa asilimia 32.5 kuhusu rasilimali ya hisa ya kawaida kuhusiana na mwaka uliomalizikia Desemba 31, 1994.
- 3 Kujadili, na ikifaa, kupitisha maazimio yafuatayo kama maazimio ya kawaida:-
 - (a) **KUAMUA** kwamba kiasi cha Rasilimali za hisa kilichokubaliwa kiongezewe kutoka hisa 10,000,000 za KShs. 5 kila moja hadi hisa 30,000,000 za KShs. 5 kila moja.
 - (b) **KUAMUA** kwamba inafaa kugeuza kiasi cha Sh.11,884,210, kikiwa sehemu moja ya akiba na kuambatana na kibali cha Halmashauri ya Rasilimali na Banki Kuu ya Kenya kwamba fedha hizo zitengwe kugawiwa wenyehisa wa kawaida katika rasilimali za kampuni mradi pesa hizo zisilipwe wenye hisa kama taslimu lakini zitumiwe kulipia kikamilifu na kwa usawa, hisa 2,376,842 na zigawiwe wenye hisa kama hao kuambatana na hisa moja kwa kila nne zikiwa miongoni mwa hisa 9,507,368 zinazomilikiwa na wenye hisa (sehemu ya hisa ipuuzwe) na kwamba hisa zitakazogawiwa wenyehisa zitafikiriwa kuwa ongezeko la rasilimali za kampuni zinazomilikiwa na kila mwenye hisa lakini si kama mapato na kwamba hisa kama hizo zitafikiriwa kuwa sawa na zinginezo za rasilimali za kampuni isipokuwa zisilipiwe mgawo wa mwisho wa mwaka wa 1994 utakaotolewa Juni 30, 1995 na hisa yo yote itakayotolewa kabla ya kutolewa kwa hisa za ziada na wakurugenzi wanapewa idhini hapa watekeleze Azimio hili.
- 4 Kutoa idhini kwa Wakurugenzi waamue ada ya Wakaguzi wa Hesabu.
- 5 Kuchagua Wakurugenzi:
Kulingana na kifungu cha 96 cha Kanuni za Kampuni, Bw. W. D. Kiboro, anajiuzulu lakini kwa sababu anaweza kugombea uchaguzi, anajitolea kusimama kuchaguliwa kuwa mkurugenzi.

Kulingana na kifungu cha 110 cha Kanuni za Kampuni, Bw. A. A. A. Ekirapa, Bw. H. H. O. Awori na Bw. W. Robinson, wanastaafu kwa zamu. Kwa kuwa Mabw. Awori na Robinson wanaweza kusimama tena, wanajitolea kuchaguliwa tena. Bw. Ekirapa hatamani kuchaguliwa.
- 6 Kujadili mambo mengine yo yote yatakayostahili.

Kwa Amri ya Halmashauri
S.G. Ogutha
Katibu

Muhimu:-

Mwanachama mwenye haki ya kuhudhuria na kupiga kura anaweza kumteua Mwakilishi (Proxy) kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi huyo si lazima awe mwanachama wa Kampuni. Ili zitumike kihalali, Fomu za Uwakilishi (Proxy Forms) zinapaswa kupelekwa katika afisi ilikoandikishwa Kampuni masaa 48 kabla ya muda uliotengwa wa Mkutano.

Machi 23, 1995

Directors' Report

The Directors have pleasure in presenting their Report and the Audited Accounts for the year ended 31st December, 1994.

Group Results:

The results of the Group for the year are as set out in full in the Profit and Loss Account on Page 18.

Dividends:

The Directors recommend the payment of a final dividend of 32.5 % on the issued Share Capital at 31st December, 1994, which, together with the interim dividend of 12.5% paid on the 11th November, 1994, makes a total of 45% in respect of the year ended 31st December, 1994.

Bonus Issue:

The Directors recommend the capitalisation of reserves of KShs. 11,884,210 by the issue of shares as fully-paid-up bonus shares to Shareholders in the proportion of one bonus share for every four shares held, subject to approval by the Capital Markets Authority and the Central Bank of Kenya.

This issue of new shares will require the increase in the authorised Share Capital of the Company.

The resolutions required to give effect to these changes will be put before the Shareholders at the Annual General Meeting and are set out in the Notice of that meeting on Page 6.

Directorate:

The present Board of the Company is as set out on page 3. Mr. W. D. Kiboro was appointed to the Board on October 6, 1994. All other Directors named have been Directors throughout the year.

Mr. W. D. Kiboro retires in accordance with Article 96 while Mr. H. H. O. Awori and Mr. W. Robinson retire by rotation in accordance with Article 110. They all, being eligible, offer themselves for re-election.

Mr. Albert A. A. Ekirapa also retires by rotation and, following his retirement on March 31, 1995, is not seeking re-election.

The Chairman:

As noted above, Mr. A. A. A. Ekirapa retires as Chief Executive of the Group on 31 March, 1995 and is not seeking re-election as a Director at the Annual General Meeting. Mr. Ekirapa joined the Nation Group in 1974 as an Executive Director and took over as Chairman and Chief Executive in 1977.

His first report to shareholders, covering an 18-month period showed a profit before tax of KShs. 11.2 million. Since then with the support of directors and staff, the Group has expanded to register a profit of KShs. 251.6 million in 1994, produced from a turnover of KShs. 1.3 billion. The Board of Directors wish to record their deep appreciation of Mr. Ekirapa's contribution as Chief Executive for the past 18 years overseeing the Group's expansion, the highlights of which have been the remarkable growth of the circulations of Nation Newspapers' publications, the steady increase in advertising market share by the Group's titles, the introduction of new publications including, most recently, The EastAfrican, in addition to the move to the new Nation Centre. Under his leadership, Nation Printers and Publishers Limited has become a major publishing force in East Africa and has witnessed a record of continued improvement in profits earned and dividends paid to its 10,000 Shareholders.

Auditors:

Coopers & Lybrand will continue in office in accordance with Section 159(2) of the Companies Act (Cap 486).

By Order of the Board,
S.G. Ogutha
Secretary

23rd March 1995

Taarifa ya Wakurugenzi

Wakurugenzi wana furaha kutoa Ripoti yao pamoja na hesabu zilizokaguliwa kuhusu mwaka uliomalizikia Desemba 31, 1994.

Matokeo ya Kundi:

Matokeo ya Kundi kuhusu mwaka ni kama yalivyoonyeshwa kikamilifu katika Akaunti ya Faida na Hasara kwenye Ukurasa wa 19.

Migawo:

Wakurugenzi wanapendekeza malipo ya mwisho ya mgawo wa asilimia 32.5 kuhusu hisa zilizotolewa kufikia Desemba 31, 1994, ambao, pamoja na mgawo wa muda wa asilimia 12.5 uliolipwa Novemba 11, 1994, unajumlisha mgawo kuhusu mwaka uliomalizikia Desemba 31, 1994 kuwa asilimia 45.

Mgawo wa Ziada:

Wakurugenzi wanapendekeza ubadilishaji wa Sh. 11,884,210 zikiwa ni akiba kuwa hisa za bonasi ili zilipwe wenye hisa kulingana na hisa moja ya bonasi kwa kila nne zinazomilikiwa. Hisa zitatolewa kulingana na idhini ya Halmashauri ya Rasilmali na Banki Kuu ya Kenya.

Kutolewa kwa hisa hizi mpya kutakuwa na maana kwamba kutakuwa na ongezeko la rasilmali za hisa za kampuni.

Azimio la kuidhinisha mabadiliko haya litapendekezewa wenye hisa katika mkutano wao mkuu kama ilivyoielezwa katika ilani ya mkutano kwenye ukurasa wa 7.

Wakurugenzi:

Halmashauri ya sasa ya Wakurugenzi ni kama ilivyoielezwa katika ukurasa wa 3. Bw. W. D. Kiboro aliteuliwa katika Halmashauri mnamo Oktoba 6, 1994. Wakurugenzi wengine walioelezwa hapo walikuwa wakurugenzi mwaka huo wote.

Bw. W. D. Kiboro atajiuzulu kulingana na kifungu cha 96 hali Mabw H. H. O. Awori na W. Robinson watajiuzulu kulingana na kifungu cha 110. Na kwa sababu wanaweza kuchaguliwa, wamejitolea tena kuchaguliwa wakurugenzi.

Bw. Albert A. A. Ekirapa kadhalika anajiuzulu lakini kufuatia kustaafu kwake mnamo Machi 31, 1995, hatasimama tena kuchaguliwa.

Mwenyekiti:

Kama ilivyoielezwa hapo juu, Bw A. A. A. Ekirapa anastaafu kama Mkuu wa Kundi kuanzia Machi 31, 1995 na hatasimama kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wakati wa Mkutano Mkuu wa kila Mwaka.

Bw. Ekirapa alijiunga na Kundi la Nation mnamo 1974 akiwa Mkurugenzi Mkuu na baadaye akawa Mwenyekiti na Mkuu mnamo 1977.

Ripoti yake ya kwanza kwa wenye hisa, iliyohusu kipindi cha miezi 18, ilionyesha faida ya Sh. 11,200,000 kabla ya kodi kukatwa. Tangu wakati huo, na kwa ushirikiano wa wakurugenzi na wafanya kazi, Kundi lilistawi na kufikia kiwango cha faida ya Sh. 251,600,000 mnamo 1994 iliyotokana na jumla ya mapato ya Shilingi bilioni 1.3.

Halmashauri ya Wakurugenzi ingependa kutoa shukrani zake kuu kwa Bw. Ekirapa kwa kazi yake njema aliyofanya tangu awe mkuu wa Kundi katika muda wa miaka 18 na kusimamia upanuzi wa kampuni. Mafanikio ya Kundi chini ya uongozi wake ni kama ustawi mkubwa wa magazeti ya Nation, ongezeko kubwa katika soko la matangazo ya magazeti na uanzishaji wa bidhaa mpya zinazochapishwa na kundi pamoja na gazeti jipya majuzi la The EastAfrican pamoja na hatua ya kuhamia Nation Centre. Chini ya uongozi wake, Nation Printers and Publishers Limited imekuwa kampuni kubwa na maarufu zaidi katika uchapishaji jimbo la Afrika Mashariki na imeshuhudia ustawi mkubwa wa faida na migawo iliyolipwa wenye hisa wake 10,000.

Wakaguzi wa Hesabu:

Kampuni ya Coopers and Lybrand itaendelea kukagua hesabu za kundi kulingana na kifungu cha 159(2) cha Sheria ya Kampuni (Ukurasa wa 486).

Kwa Amri ya Halmashauri,
S.G. Ogutha
Katibu

Machi 23, 1995

Chairman's Report



The Group

Last year, at the time of the Annual General Meeting, I referred to the challenges and problems that had faced us in the course of 1993. Your Company had, as I reported then, nonetheless performed well despite the adverse economic circumstances pertaining throughout that year. We were, however, looking with optimism at a much improved level of profitability in 1994 following the Government's relaxation on a whole range of economic controls.

It is therefore very refreshing to be able to commence the Annual Report for 1994 on an optimistic note after some years of business uncertainty characterized by rigid monetary and economic policies, acute shortages of foreign exchange, high inflation and low economic growth.

In the past two years the Government has taken very positive measures to introduce sound monetary policies and liberalize the economy. These measures have begun to show results in many areas of the

country's economy though there are still a few remaining obstacles to be removed to completely liberalize the economy. It is however, fair to pay tribute to the bold actions which the Government has already taken and which have met with such success.

I am therefore delighted to report greatly enhanced Group profit performance for the year. Your Group's pre-tax profit increased from KShs. 105.8 million in 1993 to an all-time record of KShs. 251.6 million in 1994, representing a growth of 137 percent.

The excellent results reported here are due, in addition to the improvement in the economy mentioned earlier, to the significant increase in revenues particularly from advertising. They have also been influenced by the reduction in interest charges, and by the strengthening of the Kenya shilling relative to hard currencies which have had a favourable impact on the cost of imported materials, and by the use of better quality imported newsprint in particular which not only significantly improved the yield but also contributed to a better-looking product.

The very satisfactory level of profitability, coupled with the developing stability in the Kenyan economy, means that your Group is poised to take full advantage of this healthy business environment. It now has the financial capability to pursue certain key long-term investments including the replacement of the Company's old printing plant.

Nation Newspapers Limited

Your newspaper company recorded exceptional performance in 1994. Turnover increased by more than 35 percent, as a result of a major improvement not only in advertising revenues mentioned earlier, but also in circulation revenues. Based on the growing superiority in the circulation of our English language publications, our advertising market share increased in volume terms from 45.3 percent to 50.5 percent.

On the cost side, the major factors contributing to the improvement in profits have been the reduction in interest rates and the effective and essential cost control measures introduced and maintained by management. In addition there were major savings on newsprint because of the strengthening of the Kenyan shilling. A recent surge in world demand for newsprint has, however, led to a doubling of prices so these gains will not be repeated.

A significant event for Nation Newspapers in 1994 was the successful launching, in November, of the new weekly regional newspaper - *The EastAfrican*. This development marked the realization of one of your Group's long term objectives of broadening its presence in the countries of East Africa and the region as a whole. The launch of the new newspaper coincided with the demonstration by leaders in the region of their willingness to revive the defunct East African Community. We are pleased that the new publication has been warmly received throughout East Africa and is now firmly established not only in Kenya but also in Tanzania and Uganda where editorial and commercial bureaux have been

Chairman's Report

Continued

established. Your management is responding to the confidence East Africans have shown in this important new weekly publication by seeking constant improvements in both the quality and content.

Nation Marketing and Publishing Limited

This company has three main products; the expanding *Kenya Business Directory*; a sister publication of *The East African Business Directory* serving Kenya, Tanzania and Uganda, which was launched during the year, and the re-vamped monthly tourist magazine *What's On*, which now also covers all three East African countries. All three publications made a healthy profit contribution in 1994. The Company's management has been brought under the direct control of Nation Newspapers Limited and the immediate intention is to consolidate current activities to maximize the Company's revenue base before embarking on the launch of new products or services.

Nation Carriers Limited

The transport subsidiary continues to be affected by high operating costs. Poor road conditions throughout the country have taken a heavy toll on our vehicles, resulting in high maintenance and repair bills. In the circumstances, the fleet replacement programme has had to be reviewed and replacement of vehicles is now more frequent. The regularity of vehicle breakdowns has, at times, resulted in delays and, as we do not foresee any marked improvement in the road network conditions, the Company will inevitably continue operating at a very high cost level. However, in

1995 the Company's management will, in an attempt to contain these costs, be drawn under much closer control from Nation Newspapers Limited.

Kenya Litho Limited

1994 was a difficult year for local manufacturers of consumer goods. The dwindling purchasing power resulting from rapid inflation and massive importation of cheap goods had substantial adverse impact on this sector. This inevitably led to shrinkage in the demand for packaging material. Despite this, a combination of measures of effective cost control and judicious cash management initiated in 1993 helped the Company to achieve satisfactory results for the year. Liberalization and importation of consumer goods has created an awareness of the need to improve local packaging, resulting in structural change in the way local goods are packed. Kenya Litho is therefore in the process of equipping itself to enable it to meet the changing needs of the market.

Industrial Promotion Building Limited

Your Group has a 20 percent interest in this Company which owns a number of commercial properties, including the prestigious Nation Centre and Industrial Promotion Services (IPS) building in Nairobi. In 1994 the Nation Centre was one hundred percent occupied and the Company reported a significant improvement in profits.

New Projects

New Printing Press

Shareholders may recall references in the Chairman's Reports over the past few years to the growing need to modernize our printing facilities. We have invested heavily in up-grading the Company's pre-press facilities. Our presses are now almost 20 years old and beginning to incur high maintenance costs. They need to be replaced if we are to fully meet the demands of readers and advertisers and the Company's objective of seeking constant improvement in the quality of our publications. The steady growth in the pagination of the *Nation* and *Taifa* alone demands a larger press, as does the growing demand for improved colour printing facilities. Given the present financial strength of the Group we are now confident that the Company can absorb the substantial costs involved in purchasing a new press. Work has begun on planning for the acquisition and installation of a new plant which will be sited in a new, custom-built, facility just outside Nairobi. Completion of this new project is planned for late 1996.

Television and Radio

Since the last Annual General Meeting, the Attorney General established a Press Task Force to make recommendations on Press Law and Media licensing and ownership. The Task Force has not yet released information relating to its deliberations and we are therefore awaiting the outcome of the Task Force's deliberations with interest.

Chairman's Report

In spite of recent reports and speculation, we are still hopeful the Government will liberalize the airwaves and not only permit, but actually encourage, the private sector to invest in the electronic media. As shareholders will know, your Group is keen to expand into these areas of media should conditions allow. We have submitted license applications and we are prepared to take up opportunities, should they appear.

Future Prospects

With the liberalization of the country's economy, your Group is in a strong position to consolidate its leadership in the media industry, both in Kenya and across the region. With Nation Group publications now commanding a pre-eminent leadership position in the print media market, the Group is ready for expansion into other areas of the industry and into other markets. We are very optimistic as to the future.

Dividend Proposal

The major increase in the profits of the Group justify, in spite of the significant investment plans mentioned earlier, an improvement in the return to shareholders by way of an increased dividend.

The Board of Directors has recommended a final dividend of 32.5 percent compared to 27.5 percent last year. A dividend of 12.5 percent was paid to shareholders on the 11th of November 1994, making a total dividend of 45 percent for the year (1993 - 40 percent)

Bonus Issue

In addition to the increased dividend, your Board of Directors has recommended, for your approval, a bonus issue of one fully paid-up share for every four shares held in the issued and paid-up share capital of the Group. These bonus shares will be subject to the receipt of the necessary approvals by the relevant authorities. Therefore these shares will not qualify for the dividend in respect of 1994.

Management Changes

Shareholders will have read in the Press about my retirement, on 31st March 1995, from the position of Chief Executive of your Group.

In preparation for my retirement, Mr. Wilfred Kiboro who has now succeeded me as Group Managing Director, joined the Group in February 1993 and, was appointed Managing Director of Nation Newspapers Limited, in July of the same year. He joined the Board of Nation Printers and Publishers Limited in October last year.

Prior to joining the Nation, Mr. Kiboro was Managing Director of Rank Xerox Limited. He brings to the Group a wide range of experience gained in working with major international companies over a period of close to 25 years, and enjoys the support of a solid team of well trained and tested professionals.


I would like to assure shareholders that with these management changes, your Group will be manned by a young and energetic team whose mission is to propel the Group to

greater success. I am satisfied that the Group is in good hands and its future is assured.

Our directors have had an extremely busy year and have put in many hours of work. Perhaps the greatest tribute I can pay to our directors, staff and shareholders is to acknowledge their unswerving loyalty to this Group, even at very trying times. I wish to take this opportunity to publicly acknowledge this support on behalf of management.

The high level of commitment by our managers and staff at all levels played a very significant part in the success we acknowledge today and to the results which I have been able to report. The introduction of Total Quality Management in the Group and the advancement of our information technology programme are just two developments that will enable our staff to deliver even better results from here out. Above all, both the management and staff will be in a better position to up-hold the editorial policy of the Group of being non-partisan, accurate and fair in serving the interests of all Kenyans.

I congratulate everyone of them for the excellent performance of the Group in 1994 and I thank them on my own and on your behalf.



A. A. A. EKIRAPA
Chairman

Kundi La Kampuni

Mwaka uliopita wakati wa Mkutano Mkuu wa kila mwaka, niliongea kuhusu matatizo yaliyotukabili mnamo 1993. Kampuni yenu kama nilivyotangaza wakati huo, iliwahi kufanya vyema kadiri licha ya hali ngumu ya kiuchumi iliyoonekana kote mwaka huo. Hata hivyo, tulitarajia kwamba kiwango cha faida kingeimarika mnamo 1994 kufuatia hatua za Serikali ya kulegeza masharti mengi yaliyosimamia uchumi.

Hivyo, ni jambo la kutia moyo na kuchangamsha kuanza Ripoti ya kila mwaka kuhusu 1994 kwa matumaini baada ya mashaka ya miaka mingi ya kibiashara yaliyotokana na maongozi mangumu ya kiuchumi na kifedha yaliyosababisha upungufu wa fedha za kigeni, gharama ya juu ya maisha na kuzorota kwa uchumi.

Katika miaka miwili iliyopita, Serikali imechukua hatua thabiti zenya lengo la kuimarisha maongozi sawa ya kifedha na kulegeza kabisa masharti ya kiuchumi. Hatua hizi zimeanza kuleta matokeo yafaayo katika sehemu nyingi za uchumi wa nchi hata ingawa kungali na vikwazo kadha vinavyotakiwa kuondolewa ili kulegeza kabisa masharti yanayosimamia uchumi. Licha ya hayo, ni busara kusifu Serikali kutokana na hatua za kijasiri iliyochukua na ambazo zimefanikiwa katika shabaha zake.

Hivyo, nina furaha kutangaza kwamba, faida ya Kundi iliimarika zaidi mnamo mwaka uliojadiliwa. Faida ya Kampuni yenu kabla ya kodi kukatwa iliongezeka kutoka Sh. 105,800,000 mnamo 1993 na kuvunja rekodi kwa kufikia Sh. 251,600,000 mnamo 1994 - ongezeko la asilimia 137.

Matokeo bora yaliyotangazwa hapa yalitokana na baadhi ya mambo mengine, kuimarika kwa uchumi kama ilivyoielezwa hapo awali na ongezeko la mapato hasa kutokana na uuzaji wa matangazo. Yalitokana pia na kupungua kwa viwango vya faida za mikopo, kuimarika kwa Shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu za kigeni ambako kulisaidia kupunguza gharama ya bidha zilizozagazwa kutoka ng'ambo na utumizi wa karatasi bora zaidi kutoka nje ambazo zilisaidia kuimarisha uchapishaji na kutoa bidhaa bora zaidi.

Kutokana na kuimarika kwa kiwango cha faida pamoja na hali ya uchumi wa nchi inayozidi kuimarika, Kundi lenu liko tayari kujinufaisha kikamilifu kutokana na hali hii njema kibiashara. Sasa, Kundi linaweza kutekeleza mipango kadha muhimu ya kirasilmali pamoja na ununuzi wa mitambo mipya ya uchapishaji.

Nation Newspapers Limited

Kampuni yenu ya magazeti ilifanya vyema mnamo 1994 huku faida za kabla ya kodi kukatwa zikiongezeka mara mbili unusu. Jumla ya mapato iliongezeka kwa zaidi ya asilimia 35 kutokana na ongezeko kubwa la mapato kutoka uuzaji wa matangazo kama ilivyoielezwa hapo awali. Hali kadhalika, mapato zaidi yalipatikana kutokana na uuzaji wa magazeti. Kutokana na uongozi wetu unaozidi kuimarika katika soko la uuzaji magazeti yetu ambapo ongezeko kubwa la uuzaji magazeti ya Kiingereza ilionekana katika kiwango cha

soko letu la matangazo, kiwango hiki kilipanda kutoka asilimia 45.3 hadi 50.5.

Kuhusu maswala ya gharama, mambo muhimu yaliyosababisha kiwango cha faida kikaongezeka yalitokana na kupungua kwa viwango vya faida ya mikopo na hatua thabiti zilizochukuliwa na wasimamizi kupunguza gharama. Mbali na hayo, kiasi kikubwa cha pesa kiliokolewa katika ununuzi wa karatasi za uchapishaji baada ya uhuru kutolewa wa kuagiza bidhaa kutoka nje na ambao ulitolewa wakati bei za kimataifa zilikuwa za chini nayo Shilingi ya Kenya ilikuwa na nguvu. Hata hivyo, ongezeko la mahitaji ya karatasi ulimwenguni limesababisha bei kupanda maradufu na hivyo, huenda hali hiyo isipatikane tena.

Tukio muhimu zaidi katika Nation Newspapers mnamo 1994 lilikuwa ni kuanzishwa kwa gazeti jipya la kila wiki katika jimbo - The EastAfrican, mnamo Novemba 1994. Tukio hilo liliambatana na moja ya shabaha za muda mrefu za kundi za kusambaza shughuli zake katika Afrika Mashariki na jimbo kwa jumla. Gazeti lilianzishwa wakati viongozi wa jimbo walipokuwa wakionyesha moyo wa kufufua Jumuiya ya Afrika Mashariki ililoyovunjika. Tuna furaha gazeti hili lilipokelewa kwa furaha kote Afrika Mashariki na tayari limeshika mizizi si Kenya tu, bali Tanzania na Uganda ambako tayari afisi za habari na biashara zimefunguliwa. Wakuu wa Usimamizi wanatilia manani imani iliyoonyeshwa na raia wa Afrika Mashariki katika gazeti hili na wanazidi kutafuta njia na mbinu za kuimarisha zaidi yaliyomo na hali yake.

Nation Marketing and Publishing Limited

Kampuni hii hutengeneza bidhaa tatu; Kenya Business Directory inayostawi, The East African Business Directory inayotumiwa Kenya, Tanzania na Uganda iliyoanzishwa mwaka uliopita na magazini ya kisasa ya habari za kitalii, What's On, inayohudumia pia nchi tatu za Afrika Mashariki. Bidhaa hizo tatu zilipata faida nafuu mnamo 1994. Usimamizi wa kampuni hii sasa umewekwa chini ya Nation Newspapers Limited na shabaha ya sasa ni kuimarisha shughuli zake ili kuongeza uwezo wake wa kifedha kabla ya kujishughulisha na uchapishaji wa bidhaa zingine mpya au utoaji huduma.

Nation Carriers Limited

Kampuni hii ya uchukuzi ingali inakabiliwa na gharama kubwa za shughuli. Hali mbaya ya barabara za nchi imesababisha magari yetu kuharibika mara kwa mara na hapo, kuongeza gharama ya kuyarekebisha. Kutokana na hali hiyo, mpango wa kuyabadilisha umekuwa ukichunguzwa upya na mapya yanayunuliwa haraka kuliko awali. Hali ya magari kuharibika mara kwa mara imesababisha magazeti kuchelewa na kwa sababu hatutarajii hali ya barabara iimarike haraka, ni wazi Kampuni itaendelea kukabiliwa na gharama kubwa ya shughuli. Hata hivyo, katika juhudi za kusimamia vyema gharama hizi, usimamizi wa Kampuni hii mnamo 1995 utatolewa zaidi kutoka Nation Newspapers.

Kenya Litho Limited

Mwaka wa 1994 ulikuwa wa shida nyingi kwa kampuni za utengeneza bidhaa nchini.

Gharama kubwa ya maisha ilisababisha upungufu wa ununuzi na hali kadhalika, uingizaji mkubwa nchini wa bidhaa za hali ya chini ulitaziti sana shughuli za viwanda hivi. Hali hii ilisababisha upungufu wa mahitaji ya bidhaa za kupakia. Licha ya hayo, hatua mbali mbali zilizochukuliwa na wasimamizi wa Kampuni za kusimamia gharama na utumizi wa busara katika shughuli za fedha mnamo 1993, ulisaidia Kampuni kupata matokeo ya kuridhisha mwaka uliojadiliwa. Ulegezaji wa masharti ya kiuchumi pamoja na uingizaji wa bidhaa za kigeni umewezeshwa viwanda kufahamu umuhimu wa kuimarisha mbinu za upakiaji bidhaa nchini. Kenya Litho inajitayarisha kukabiliana na badiliko la mahitaji ya upakiaji.

Industrial Promotion Building Limited

Kundi hili linamiliki asilimia 20 ya Kampuni hii ambayo inamiliki majumba kadha ya kibiashara pamoja na jumba la kisasa la Nation Centre na IPS Building mjini Nairobi. Mnamo 1994, jumba la Nation Centre lilipangishwa lote na Kampuni iliweza kupata kiwango nafuu cha faida.

Mipango Mipya

Mashine mpya ya uchapishaji

Wenye hisa watakumbuka ripoti za Mweyekiti za miaka iliyopita ambapo aliongea kuhusu haja ya kununua mashine mpya za uchapishaji. Tumetumia kiasi kikubwa katika ununuzi wa mitambo mingine mpya ya uchapishaji. Hata hivyo, mashine zetu kuu za uchapishaji sasa zinakaribia miaka 20 tangu zinunuliwe na zinatumiwa kiasi kikubwa cha pesa katika urekebishaji. Mpya zinahitaji

zinunuliwe ikiwa tutatosheleza mahitaji ya wasomaji na watangazaji pamoja na shabaha za Kampuni za kuendelea kuimarisha hali ya magazeti na bidhaa zetu. Ongezeko la kurasa katika magazeti ya Nation na Taifa pekee yanahitaji mashine kubwa zaidi za uchapishaji kama vile kuna mahitaji zaidi ya uchapishaji wa rangi. Kutokana na uwezo wa sasa wa kifedha wa Kundi, tuna imani kwamba Kampuni inaweza kugharamia ununuzi wa mashine mpya ya uchapishaji. Kazi imeanza ya kununua na kuweka mashine mpya ambayo itawekwa katika jumba letu la kisasa litakalojengwa kiungani tu mwa Nairobi. Mpango huu unatarajiwa kukamilishwa mwishoni mwa 1996.

Televiseni na Redio

Tangu Mkutano Mkuu wa Mwaka uliomalizika, Mkuu wa Sheria aliteua kamati ya kuchunguza sheria zinazohusu uandishi ili itoe mapendekezo kuhusu sheria ya uandishi na utoaji leseni kwa vyombo vya utangazaji na umilikaji. Kamati hii haijataoa habari kuhusiana na shughuli zake. Kadiri tujuavyo, kamati hii, kulingana na ilivyopangiwa, haijasafiri kutoka nje ya Nairobi wala haijatafuta maoni kutoka kwa wananchi kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa taratibu zake za kikazi. Hivyo, tunasubiri matokeo ya shughuli za kamati hii kwa hamu.

Licha ya ripoti na uvumi wa majuzi, tunaamini kwamba wakati utawadia ambapo Serikali italegeza masharti yake kuhusu utangazaji lakini si kuruhusu tu, bali kutia moyo mashirika ya kibinafsi kuweka rasilimali katika shughuli za utangazaji. Kama wenye hisa

Taarifa ya Mwenyekiti

wanavyojua, Kundi lenu lina hamu ya kushiriki katika shughuli hizi za usambazaji habari iwapo hali itawezesha. Tumepelekea Serikali maombi ya leseni na tuko tayari kuanza shughuli ikiwa nafasi itatolewa.

Matumaini ya Baadaye

Kufuatia kulegezwa kwa masharti ya kibiashara, Kundi lenu liko tayari na liko katika hali njema ya kuimarisha umaarufu wake katika shughuli za uenezaji habari nchini Kenya na kote jimboni. Na kwa sababu magazeti ya Kundi la Nation yanaongoza katika soko la magazeti, Kundi sasa liko tayari kupanua shughuli zake katika sehemu zingine za kiwanda na masoko mengine. Tuna matumaini makubwa kuhusu hali ya baadaye.

Mapendekezo ya Mgawo

Ongezeko kubwa la faida za Kundi lina maana kwamba, licha ya mipango ya kirasilmali iliyoolezwa hapo awali, wenye hisa wanastahili mapato nafuu katika nyongeza zao za mgawo.

Halmashauri ya Wakurugenzi inependekeza mgawo wa mwisho wa asilimia 32.5 ukilinganishwa na wa asilimia 27.5 ulitolewa mwaka uliopita. Mgawo wa asilimia 12.5 ulilipwa wenye hisa mnamo Novemba 11, 1994, na hapo, kujumlisha mgawo wa mwaka huo kuwa asilimia 45 (1993 - asilimia 40)

Toleo la Bonasi

Pamoja na mgawo ulioongezwa, Wakurugenzi wamependekeza, ili mtoe idhini, toleo la bonasi ya hisa moja iliyolipwa kikamilifu kwa kila

hisa nne zinazomilikiwa na zilizolipwa katika rasilimali za hisa za Kundi. Hisa hizi za bonasi zitalipwa kutegemea idhini inayotakikana ya walio mamlakani. Hiyo, hisa hizi hazitahesabika kwa mgawo kuhusiana na 1994.

Mabadiliko Katika Usimamizi

Wenye hisa watakuwa wameshasoma magazetini kuhusu kustaafu kwangu mnamo Machi 31, 1995, kutoka cheo cha Mkuu wa Kundi lenu.

Katika kujitayarisha kustaafu, Bw Wilfred Kiboro, ambaye sasa anachukua mahali pangu akiwa Mkurugenzi Mkuu wa Kundi, alijiunga na Kundi mnamo Februari 1993 na aliteuliwa Mkurugenzi Mkuu wa Nation Newspapers Limited mnamo Julai mwaka huo. Alijiunga na Halmashauri ya Wakurugenzi wa Nation Printers and Publishers mnamo Oktoba mwaka uliopita.


Kabla ya kujiunga na Nation, Bw Kiboro alikuwa Meneja Mkurugenzi wa Rank Xerox Limited. Anajiunga na Kundi akiwa na ujuzi mwingi aliopata akifanya kazi katika mashirika ya kimataifa katika kipindi cha karibu miaka 25 na anaungwa mkono na kundi la wafanya kazi wenye ujuzi na waliofunzwa kikamilifu.

Ningependa kuwahakikishia wenye hisa kwamba kutokana na mabadiliko haya, Kundi lenu litasimamiwa na watu wachanga na wenye moyo wa kuendeleza Kundi katika ufanisi zaidi. Nimeridhika kwamba Kundi liko mikononi mwa watu wenye uwezo na hali ya baadaye ina matumaini makubwa.

Wakurugenzi wenu wamekuwa na shughuli nyingi mwakani na walifanya kazi kwa masaa mengi. Pengine shukrani kuu ninazoweza kuwapa wakurugenzi wetu, wafanya kazi na wenye hisa ni kushukuru kutokana na imani yao kubwa katika Kundi hili hata nyakati za shida nyingi. Kwa niaba ya wasimamizi, ningependa kutangaza shukrani zangu kutokana na imani hii.



